OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA

TAARIFA YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI MKUTANO WA KAWAIDA WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 12/08/2022 KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA NNE MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

- Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Siha,
- Mwakilishi Ofisi ya RAS-Mkoa wa Kilimanjaro,
- Mh. Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Siha,
- Mhe. Makamu Mwenyekiti Halmashhauri ya Siha
- Waheshimiwa Madiwani,
- Ndugu Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Siha (Katibu wa Baraza),
- Wah Viongozi wa Madhehebu ya Dini,
- Wageni Waalikwa,
- Ndugu Wataalamu,
- Waandishi wa Habari,
- Wananchi wa Wilaya ya Siha,
- Mabibi na Mabwana,

Nawasalimu wote kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipekee napenda kumshukuru Mungu sana kwa ajili ya mshikamano na umoja unaoendelea kuimarika kila siku kati ya Viongozi na Wananchi,Pia kati ya Wananchi na Wananchi pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Siha.

Mshikamano huu siyo wa kawaida bali ni upendeleo tu tumepata kutoka kwa Mungu wetu kwani tumeona na kusikia jinsi maeneo mengine wanavyovurugana na kukosa maelewano.

Aidha, kwa namna ya kipekee napenda kutoa shukrani za dhati kwa Serikali yetu ya awamu ya Sita inaongozwa na **mhe.SAMIA SULUHU HASSAN** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyofanya juhudi kubwa ya kuipatia fedha nyingi za maendeleo Halmashauri yetu ya Wilaya ya Siha ambazo fedha hizo zinatumika kuboresha utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Vile vile napenda kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi (CCM) kwa jinsi kinavyoendelea kusimamia Serikali iliyopo madarakani na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora tena kwa wakati.

Aidha, napenda pia kuwashukuru **Wah. Madiwani wote** wa Halmashauri ya Siha kwa ushirikiano wenu wa dhati na jinsi mnavyoshiriki katika ubunifu na usimamizi ulio bora wa uendeshaji wa Halmashauri ya Siha hususani katika kuhamasisha shughuli za maendeleo katika Kata.

Wah. Madiwani , na Ndugu Wananchi,

Katika Kipindi hichi cha robo ya Nne Wilaya yetu ilipokea ugeni mkubwa wa **Mhe. Dkt.Philip Isdor Mpango** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipofika katika Hospital ya Taifa ya Magonjwa ambukizi **Kibong'oto tarehe 16.07.2022** kwenye tendo la ufunguzi wa maabara ya kisasa katika Hospital hiyo. napenda kuwashukuru Viongozi wote wa chama na Serikali waliofanikisha mapokezi hayo muhimu katika Wilaya yetu.

Wah. Madiwani , na Ndugu Wananchi,

Katika taarifa yangu kwa kipindi cha Robo ya Nne yapo mambo muhimu nimeona niyazungumzie kama sehemu ya kusisitiza katika kipindi husika na kijacho. Miongoni mwa masuala machache yaliyopo katika taarifa yangu ni pamoja na suala la **Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya**

Halmashauri,Utekelezaji Miradi ya Maendeleo,Utunzaji wa Chakula pamoja na Utendaji kazi wa Halmashauri ya Siha.

A. UKUSANYAJI WA MAPATO

Waheshimiwa Madiwani, Ndugu Wananchi

Kwanza Kabisa napenda kutoa pongezi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Siha pamoja na Wataalam kwa juhudi kubwa waliyofanya ya kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Siha kwa zaidi ya asilimia **115.76** katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Kiukweli Mkurugenzi Mtendaji pamoja na timu yako Umetupa heshima kubwa sana Halmashauri yetu kwa uchapakazi wako wa kusimamia zoezi la ukusanyaji wa mapato na pia katika kusimamia vema matumizi sahihi ya fedha za Umma.

Pamoja na pongezi hizi nyingi tulizowapatia, Naomba juhudi zaidi ziendelee kufanyika katika mwaka mpya wa fedha **2022/2023** ulioanza mwezi Julai katika kuhakikisha kuwa mapato ya Halmashauri yanakusanywa katika viwango vinavyotakiwa na kubuni vyanzo vipya vya mapato kama ilivyo mapendekezo ya **Wah. Madiwani**.

Naomba kuendelea kurudia kutoa msimamo wa baraza la Wah Madiwani kuwa,Sisi kama baraza la Madiwani katika Halmashauri ya Siha hatutakuwa tayari kuona mtu yeyote anatumia fedha za Serikali vibaya na atakayebainika kuhujumu na kutumia fedha za Serikali kwa maslahi yake binafsi basi hatua stahiki zitachukuliwa dhidi yake, Ndugu zangu wataalam na wote mliopewa dhamana na Serikali tumeona tuyaseme haya mapema ili baadaye wakati wa utekelezaji kila mtu atimize wajibu wake.

B. UTUNZAJI WA CHAKULA

Wah. Madiwani na Ndugu Wananchi

Kama mnavyojua ndugu zangu Wananchi na Wakazi wa Wilaya ya Siha kuwa msimu wa kipindi cha masika kwa mwaka huu haukuwa mzuri na hivyo upatikanaji wa mazao ya chakula huenda usiwe katika viwango tulivyovizoea.

Naomba kutoa wito kwa Wah.Madiwani na Viongozi wengine tuendelee kuwapa elimu ya kutosha wananchi wetu kutunza chakula kitakachopatikana wakati wa mavuno. Jambo hili nimeona nitoe msisitizo wa kutosha kwani hatuwezi kupata maendeleo iwapo wananchi wetu watapata uhaba wa chakula. Naomba kutoa wito kwa Mkurugenzi Mtendaji

awajulishe Watendaji wa Vijiji na Kata katika maeneo yetu ili watusaidie kufikisha ujumbe huu kwa wananchi na Wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha

C. UTENDAJI KAZI WA HALMASHAURI YA SIHA

Waheshimiwa Madiwani,Ndugu Wananchi

Wah. Madiwani na Wajumbe wa Baraza la Madiwani kwa ujumla Halmashauri yetu imeendelea kufanya vema katika utendaji kazi hususani utoaji wa huduma bora kwa Wananchi pamoja utekelezaji na usimamizi wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Ndugu zangu tarehe **02/08/2022** mneona na kusikia taarifa iliyotolewa na **Mhe.Innocent Bashungwa (Mb)** Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tamisemi ikionesha matokeo ya ujumla ya utendaji kazi na usimamizi bora wa Halmashauri hapa nchini kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Juni 2022.

Katika Taarifa hiyo Halmashauri yetu ilikuwa katika nafasi 10 bora ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Siha imeshika nafasi ya 6 na kuwa miongoni mwa Halmashauri iliyofanya vizuri katika uendeshaji bora wa Halmashauri hapa nchini huku baadhi ya vigezo muhimu vilivyozingatiwa ikiwa ni

pamoja na Ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri,utoaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake,Vijana na Watu wenye Ulemavu,Pia upelekaji wa fedha za mapato ya ndani asilimia 40 katika miradi ya maendeleo,upunguzaji wa hoja katika Taasisi pamoja na matumizi sahihi ya fedha za Umma kwa kuzingatia sheria,Taratibu na Miongozo ya Serikali.

Naomba tena kwa niaba ya Baraza la Madiwani nitoe pongezi nyingi kwa Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Timu yake kwa mafanikio haya makubwa kwa Halmashauri yetu. Pia napenda kumpongeza **Mhe. Thomas Apson** Mkuu wa Wilaya ya Siha kwa usimamizi na ufuatiliaji wa uendeshaji wa Halmashauri.

Aidha,Kipekee napenda kumshukuru Mhe. **Dkt. Godwin Mollel** Naibu Waziri wa Afya na Mbunge wa Jimbo la Siha kwa ushauri na ufuatiliaji wake wa fedha za maendeleo katika Halmashauri yetu. Pia nawashukuru Wah.Madiwani wote kwa ushirikiano wenu na uchapakazi wenu uliotukuka wa kusimamia vema Halmashauri ya Siha.

D. MIRADI YA MAENDELEO

Wah. Madiwani ,Viongozi na Ndugu Wananchi

Katika Utekelezaji wa miradi ya maendeleo Halmashauri yetu imeendelea kupokea fedha nyingi kutoka Serikali kuu ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 tumepokea zaidi ya shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kipekee kama Baraza la Wah. Madiwani tunatoa pongezi na shukrani nyingi kwa **Mhe. Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuinua maisha ya Watanzania hasa wananchi wa kipato cha chini.

Aidha,katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 Halmashauri yetu imetoa na kupeleka fedha za makusanyo ya ndani katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kiasi cha zaidi ya shilingi **milioni 455.14** ambayo ni sawa na zaidi ya asilimia 99 ya lengo kwa mwaka. Wah Madiwani hii ni hatua na juhudi kubwa zinazofanywa na Halmashauri yetu chini ya Mkurugenzi Mtendaji na Timu yake. Naomba kutoa rai kwa Mkurugenzi Mtendaji kwa juhudi hizi pia ziendelee katika mwaka wa fedha 2022/2023 ili halmashauri yetu iendelee kung'aa zaidi hapa Kilimanjaro na Taifa kwa ujumla.

Waheshimiwa Madiwani na Ndg Wananchi

Kabla sijahitinisha taarifa yangu napenda kutoa pongezi tena kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Siha kwa kufanya maandalizi mazuri na kufanikisha ziara ya kujifunza Wah Madiwani katika maonesho ya Nane nane kwa mwaka huu 2022 ambayo yanahusisha kilimo,mifugo na uvuvi ambapo Wah Madiwani walishiriki tarehe 7/8/2022. Katika Maonesho hayo ya nane nane Halmashauri yetu imefanya vizuri kwa kupata tuzo ya kutoa mfugaji bora wa ng'ombe na kondoo na hivyo kuleta heshima kubwa kwa taasisi yetu.Napenda kumpongeza mfugaji wetu **Daud Dapash Mollel** kutoka Kijiji cha Namwai Kata ya Ngarenairobi.

Napenda pia kuwashukuru Wah. Madiwani wote,Viongozi mbalimbali ndani ya Wilaya ya Siha pamoja na Wananchi kwa ujumla kwa jinsi mlivyoshiriki katika mapokezi ya Mwenge wa Uhuru tarehe **12.6.2022** ulifika na kukimbizwa katika maeneo mbalimbali ya Wilaya yetu. Kama mnavyojua Mwenge wa Uhuru wa Mwaka huu ulikuwa mgumu kwani wenzetu wa maeneo mengine wamepata shida kwa baadhi ya miradi ya maendeleo kukataliwa kuwekwa mawe ya msingi,kufunguliwa au kuzinduliwa lakini kwa maombi yenu wote sisi Halmashauri ya Siha tumevuka salama katika

miradi yetu yote iliyotembelewa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2022. Kipekee tunamshukuru Mkuu wetu wa Wilaya pamoja na Mbunge wetu kwa jinsi wanavyoendelea kushirikiana na uongozi wa Halmashauri katika usimamizi bora wa miradi ya maendeleo.

wah Madiwani ,ndugu Wananchi

Mwisho lakini siyo kwa umuhimu, wote tunajua kuwa taifa letu kwa sasa lipo katika maandalizi ya sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Nchi nzima na katika Wilaya yetu pia tarehe 23.8.2022. Naomba kutoa wito kwa Wah. Madiwani pamoja na Watendaji wa Kata na Vijiji tuendelee kuwakumbusha wakazi na wananchi wa Siha kushiriki vema katika sensa ya watu na makazi mwaka huu kwa maendeleo ya Taifa letu. Najua kwa sasa wale wenye sifa waliopata ajira ya muda wanaendelea na mafunzo kwa ajili ya kufanikisha zoezi hilo.

Mwisho kabisa na kwa namna ya pekee nawashukuru wananchi wangu wa Kata ya Karansi kwa jinsi wanavyoendelea kuniamini na kuniombea afya njema katika nafasi yangu ya Udiwani,Napenda kuwaambia kuwa sintawaangusha.

Vilevile nawashukuru tena Wah. Madiwani wenzangu pamoja na Watumishi wa Serikali katika Halmashauri ya Siha kwa jinsi mnavyochapa kazi kwa kujituma,naomba ushirikiano uliopo uendelee daima siku zote kwa maendeleo ya Wananchi wa Wilaya ya Siha. Nawashukuru pia Wananchi na Wakazi wa Siha kwa usikivu wenu mkubwa mlionesha tangu mwanzo wa taarifa yangu hadi sasa ninapohitinisha taarifa yangu, naomba usikivu na utulivu huu uendelee hadi mwisho wa Mkutano wetu.

Mungu ibariki Tanzania,Mungu ibariki Wilaya yetu ya Siha

Asanteni sana kwa kunisikiliza

Imetolewa na:

Mhe. Duncan B. Urassa

Mwenyekiti wa Halmashauri (W)

SIHA

Jiandae kuhesabiwa siku ya Jumanne 23 Agosti,2022